JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME

SHULE YA SEKONDARI SIRARI,
S.L.P. 337,
TARIME.

Kumb. Na. SSS/JIF/F.1/2021 11/12/2020.

Ndugu……

Mzazi/Mlezi wa…….

S.L.P……..

YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI SIRARI

Nafurahi kukujulisha kwamba, Mwanao…..... amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Sirari mwaka 2021. Mwanao ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliofaulu na kuchaguliwa kujiunga na shule hii ya Sirari Sekondari. Uongozi wa Shule kwa niaba ya BODI ya shule na walimu wote wanampa **HONGERA SANA**.

Kwa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza, Mzazi/Mlezi unapaswa kuhakikisha kwamba mwanao anatumia nafasi hii vizuri na anafaulu kuendelea na masomo ya juu baada ya kuhitimu. Dhima yetu ni **ELIMU-SILAHA DHIDI YA UJINGA NA UMASIKINI**. Hivyo, msimamie, msisitize ili Elimu atakayoipata iweze kumsaidia.

Aidha, unaombwa kutoa **ushirikiano** kwa uongozi wa shule katika **kumuasa** mwanao kuepuka vitendo viovu vitakavyo mharibia mwelekeo wa masomo yake, na wewe mwenyewe **usiwe kikwazo** cha maendeleo yake kwa kushindwa kumnunulia sare za shule na sare za michezo kama ilivyoelekezwa katika barua hii.

1. JIOGRAFIA YA SHULE

- Shule ya Sekondari Sirari ni ya kutwa (Day School) na ya mseto (Wavulana na Wasichana)
- Shule ipo katika Kata ya Sirari, Tarafa ya Inchungu Wilaya ya Tarime.
- Shule ipo takribani KM 1.5 kutoka Sirari mpakani na Meta 700 kutoka Barabara kuu iendayo Mwanza upande wa kulia, kibao (Signboard) kipo kinaonekana.

2. KURIPOTI

Shule itafunguliwa siku ya Jumatatu tarehe **11/01/2021**. Hii ndiyo siku **anayotakiwa pia kuripoti** mwanafunzi, na mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe **22/01/2021**, hivyo unatakiwa kumuandaa mwanao na afike na mahitaji **yote** yaliyoelezwa kwenye fomu ya maelekezo. Siku atakayoripoti mwanafunzi lazima afike na barua hii ya maelekezo ya kujiunga na Shule. **NI KOSA** kumpa au kumuuzia barua hii ya maelekezo/nafasi mtu mwingine ambaye hakufaulu/hausiki. **TSM 9** ya mwanafunzi aliyefaulu itatumika kuhakiki uhalali wa mwanafunzi siku atakayoripoti.

3. MAAGIZO KWA MWANAFUNZI

3:1 MASOMO

Mwanafunzi atalazimika kusoma masomo tisa (9) ambayo ni **Civics**, **English**, **Geography**, **History**, **Kiswahili**, **Biology**, **Physics**, **Chemistry** na **Basic Mathematics**.

Masomo yote hufundishwa kwa Lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili tu. Ili kuyamudu, Mwanafunzi atalazimika kuongea Kiingereza muda wote awapo shuleni nje na ndani ya Darasa. Majuma nane ya mwanzo tangu kufungua Shule, wanafunzi watafundishwa vipindi maalum kwa kiingereza (Orientation Course).

3:2 VIFAA VYA DARASANI

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo siku ya kuripoti.

- Madaftari makubwa (Counter book quire 2) yasiyopungua kumi (10).
- Mathematical Set, Kalamu, Penseli na Rula.
- Begi la kubebea Madaftari.
- Ream (Double A) kwa ajili ya mazoezi ya mwanafunzi

3:3 SARE ZA SHULE

- Sketi na Suruali, Wanafunzi watashona kitambaa **nyeusi**. Tafadhali zingatia ubora. (Material).
- Sweta rangi ya **Bluu**.

A. WASICHANA

- Sketi mbili ndefu zilizovuka magoti **(Linda Box)**. Sketi vimini, ni **marufuku** kwa muda wowote wa masomo wa miaka minne mwanafunzi atakao kaa shuleni.
- Blauzi **nyeupe** mikono mifupi mbili.
- T. Shirt rangi ya **blue bahari** yenye nembo ya shule itakayovaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa.
- Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofungwa kwa kamba.
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili
- **Track suit rangi ya bluu bahari na raba kwa ajiri ya michezo,** zitavaliwa siku na muda wa michezo tu.
- Hijab kwa Waislamu (Suruali rangi ya kitambaa cha sare ya Shule na Gauni /Kanzu nyeupe)

B. WAVULANA

- Suruali mbili zenye mifuko mitatu na marinda mawili tu kila upande, zisishonwe kwa madoido/mitindo ya kihuni kama **Piston**, **Modo** na isiburuze chini. **KAMWE** isivaliwe kwenye matako stahili ya **'Kata K'**
- Mashati meupe yenye mikono mifupi mawili.
- T. Shirt rangi ya **blue bahari** yenye nembo ya shule itakayovaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa.
- Soksi rangi nyeusi au dark blue jozi mbili.
- **Track suit rangi ya bluu bahari na Raba kwa ajiri ya michezo**, zitavaliwa siku za michezo tu.

NB:

-Raba ni kwa ajili ya michezo tu, viatu vya wazi, kandambili haviruhusiwi kabisa.

-Muda wote mwanafunzi anapokuwa shuleni anapaswa kuvaa sare za Shule, kuonekana msafi na nadhifu, hivyo awe na sare za shule za kubadilisha.

-Masweta yasiyo sare, Majaketi na Makoti hayaruhusiwi kabisa hivyo mwanafunzi asije nayo ili kuepuka adhabu zisizo za lazima.

4. FOMU MAALUMU

-Zijazwe kama zinavyojieleza

-Hati ya uthibitisho wa afya ya Mwanafunzi ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali/kituo cha Afya cha Serikali.

NB: <u>Kila mwanafunzi aje na kopi ya cheti cha kuzaliwa</u>.

5. SHERIA ZA SHULE

Fomu iliyo na Sheria za Shule imeambatanishwa, Mwanafunzi azisome kwa makini na azizingatie na asaini ili kuonyesha kukubaliana nazo. Mzazi pia asaini fomu ya Sheria hizo kabla ya kumleta mtoto shuleni.

6. MWISHO

<u>Kwa Mawasiliano</u>:

- Mkuu wa Shule (1) 0784-549494
  (2) 0762-310610
- Makamu Mkuu wa Shule (1) 0627-453949
  (2) 0768-405107

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

Bulogo Stephen Mbeba
<u>MKUU WA SHULE</u>

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI SIRARI S.L.P. 337 – TARIME

SHERIA ZA SHULE

1. Fuata taratibu na maelekezo yote yatolewayo shuleni.
2. Usiwe nje ya mipaka ya Shule bila **ruhusa ya maandishi** kutoa kwa mwalimu wa zamu.
3. Uwe na heshima na utii kwa viongozi wote pamoja na wananchi kwa ujumla.

MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA MAMBO YAFUATAYO

4. Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na kufuga ndevu.
5. Kuvaa mavazi yasiyo sare rasmi ya shule ndani ya eneo la shule muda na siku za shule.
6. Kuiga mitindo ya kihuni/isiyofaa kama kuvaa mitepesho/milegezo, kuvaa vimini na vitopu, kuchora matatu mwilini nk.
7. Kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia madawa.
8. Kutembelewa na wageni muda wa vipindi.
9. Usifanye makosa yafuatayo kwani yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule:-
    a) Wizi
    b) Uasherati na Ushoga
    c) Ubakaji
    d) Ulevi na Matumizi ya Madawa ya kulevya kama vile uvutaji Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na Kadhalika.
    e) Kupigana au Kupiga.
    f) Kuharibu kwa makusudi Mali ya Umma.
    g) Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
    h) Kuwa mjamzito/Kupata mimba au kusababisha mimba.
    i) Kuoa au Kuolewa.
    j) Kutoa Mimba.
    k) Kugoma, kuchochea, na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
    l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
    m) Kuwa na simu ya mkononi, kamera au redio shuleni.
    n) Utoro/kutofika shuleni bila taarifa ya mzazi/mlezi.
    o) Kuja na silaha ya aina yoyoye shuleni (Sime, Panga, Kisu, Rungu nk)
    p) Kuja shuleni na usafiri wa pikipiki/Bodaboda
    q) Tumia Lugha ya Kiingereza wakati wote wa masomo
    r) Udanganyifu katika mitihani yoyote hapa shuleni.

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME
SHULE YA SEKONDARI SIRARI

TAARIFA YA MWANAFUNZI

1. Majina Kamili ya Mwanafunzi……..

2. Jina la Mzazi/Mlezi……

3. Kama ni Mlezi/Uhusiano……Namba za Simu……..

4. Anwani ya Kudumu ya Mzazi/Mlezi…….

5. Mahali Mwanafunzi alipozaliwa: Kijiji cha……Kata ya……..
   Wilaya ya……...Mkoa wa……

6. Dini…….Dhehebu…….

7. Kutoka Shule ya Msingi……..Wilaya ya…….....
   Mkoa wa …….

8. Ndugu wengine wanaoweza kupelekewa taarifa zako muhimu za masuala ya shuleni:-
   i)……Uhusiano……..Namba za Simu…….
   ii)……Uhusiano……..Namba za Simu……..
   iii)……Uhusiano……..Namba za Simu……..

9. Kabla hujaja hapa shuleni umepimwa na Daktari? NDIYO/HAPANA. Ni ugonjwa upi ni wa kudumu kwako?.....

10. Sifa Maalumu kama unazo……...

11. Taarifa za Wazazi: Wapo wote……...yupo mmoja…….Wamefariki…….....
    (Weka alama ya vema panapohusika).

MAELEZO YALIYOPO HAPO JUU NI SAHIHI

…… ……

SAINI YA MWANAFUNZI **SAINI YA MZAZI/MLEZI**

AHADI YANGU MIMI (Jina la Mwanafunzi)…….....nakubali kwa dhati kabisa nafasi hii niliyopewa na Taifa kujiunga na Shule hii. Naahidi kufuata sheria za Shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na Uongozi wa Shule.

MIMI MZAZI/MLEZI (Jina)……nimeyasoma masharti na Sheria za Shule ya Sekondari Sirari ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanangu kufuata taratibu na sheria zote za Shule. Aidha naahidi kushirikiana na Uongozi wa Shule katika kutoa maelekezo bora kwa mwanangu ili baadae awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

Tarehe……

Saini ya Mwanafunzi…….

Jina la Mwanafunzi……

Tarehe…….

Saini ya Mzazi/Mlezi…….

Jina la Mzazi/Mlezi……

NB: Mwanafunzi ambayeatakuwa Mtoro bila sababu za msingi Mzazi/Mlezi Wake atashitakiwa kwa mujibu wa Sheria.

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT MEDICAL

CERTIFICATE

(To be completed by a medical Officer in Government Hospital in respect of all entrants to Sirari Secondary School)

Pupil's full name ……

Age ……..

1. Blood count (red and white) ……
2. Stool examinations ……
3. Urinalysis ……
4. Syphilis test ……
5. T.B. test ……..
6. Eye test ……
7. Ears test ……..
8. Chest ……
9. Abdomen ……
10. Spleen ……...

11. Additional information: e.g. physical defect, infection, chronic or family diseases etc
    ……
    ……
    ……

    Treatment after examination…….
    …….
    ……..
    (Please state nature of treatment)

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further studies

Signature ……

Designation ……

Station ……..

Date: …… Official stamp …….